# Michakato wa Elimu Maalumu: Unachohitajika Kufahamu

Kama mzazi wa mtoto anayepokea elimu maalumu, ni muhimu kusoma na kuelewa dhana muhimu ili uweze kuwa mtetezi mzuri wa elimu ya mtoto wako. Vipengele muhimu vinavyozungumziwa katika mwongozo huu ni pamoja na:



- Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (IDEA)
- Maana ya Elimu Maalumu
- Mchakato wa Elimu Maalumu
- Haki za Kufuata Utaratibu
- Je, Unahitaji Usaidizi Zaidi?

## Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (IDEA)

Kwa hisani ya sheria ya kitaifa iitwayo
Sheria ya Elimu kwa Watu Walemavu, au (IDEA), watoto wenye ulemavu wana haki ya kupata elimu ya umma ya bure. Hii inamaanisha kwamba elimu maalumu na huduma zinazohusiana vipo kwa watoto wenye ulemavu wanaohitaji wenye miaka 3 hadi 22 na bila malipo yoyote kutoka kwa wazazi. Sheria hii inawa wazazi fursa na haki ya kuwa mwanachama wa timu inayofanya maamuzi kuhusu elimu ya mtoto wako. Kwani mzazi una haki ya:

- Kupashwa habari (kimaandishi, katika lugha yako ya mwanzo) au kinga za kiutaratibu (haki za kisheria) zilizopo kwa ajili yako
- Kupokea nakala za haki hizi katika kipindi fulani katika mchakato kutoka shuleni.

## Maana ya Elimu Maalumu

IDEA inaelezea 'Elimu Maalumu' kama mafunzo mahususi yaliyopangiwa, bila malipo kwa mzazi, ambaye ana sifa za mahitaji maalumu kwa mtoto mwenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na:
Madarasa ya kawaida na maalumu

- Shule maalumu
- Mafunzo ya mazoezi ya viungo
- Mafunzo ya nyumbani
- Hospitali na taasisi
- Mafunzo ya ufundi



## Mchakato wa Elimu

Mchakato wa elimu maalumu umeundwa kuhakikisha kwamba kila mtoto mwenye ulemavu atapata elimu inayomlenga yeye ili aweze kufikia mahitaji yake. Ni muhimu kuelewa kwamba mchakato huu una sehemu nyingi na kusoma kila sehemu in muhimu.
Michoro ifuatayo inaonyesha kikamilifu yanayotendeka katika mchakato. Itumie kama mwongozo kwa sababu kila sehemu itafafanuliwa hapa chini.

### *Rufaa/Kupatikana kwa Mtoto:*

Kama mtoto wako anapata matatizo shuleni, anaweza kupewa rufaa ya kutathminiwa kwa ajili ya elimu maalumu. Rufaa hii inaweza kutoka kwako wewe kama mzazi, shule au mtoto wako. Hakikisha kwamba kama wewe mzazi ndiye unaomba tathmini, ombi lako liko katika maandishi na linafafanua mashaka yao. Hili linasaidia kujua kama elimu yao inaathiriwa kihasi na ulemavu. Matokeo ya rufaa yanayotegemewa ni:

- Shule itachukua hatua ya kuanza mchakato wa tathmini.
- Shule itaamua kwamba tathmini haihitajiki.

Haijalishi kama watasonga mbele na tathmini au la, shule lazima iwape wazazi uamuzi kwa njia ya maandishi ujulikanao kama (ilani ya mapema ya maandishi) ikiwa na maelezo juu ya uamuzi uliochukuliwa.

### *Tathmini:*

Tathmini ni mchakato wa kukusanya taarifa kuhusu mtoto ambazo zitatumika kufanya maamuzi ya kustahiki upewaji wa elimu maalumu. Mtoto atafanya mfululizo wa mijarabu inayolenga maeneo yake ya masomo kama vile stadi za lugha, elimu ya darasani, jamii, hisia, ufahamu na matokeo ya kiafya. Baadhi ya vitu muhimu vya kukumbukwa ni:

- Shule huwa na muda wa siku 45 kukamilisha mijarabu mara tu mzazi ametoa ruhusa kimaandishi.
- Unaweza kushiriki na tathmini zozote, ulemavu wowote uliopatikana na matatizo unayoyaona nyumbani.
- Lazima mtoto apewe mjarabu katika lugha yao ya mwanzo na ajaribiwe katika maeneo yote penye mashaka.

## *Kustahiki (Kuainishwa):*



Wanafunzi wanaochukuliwa kuwa wanastahiki huduma za elimu maalumu lazima wafikie 3 ya vigezo vilivyooneshwa katika mchoro huu. Timu (wakiwemo wazazi) wanahakiki takwimu za tathmini kuaua kama mwanafunzi anaonyesha ulemavu katika 1 ya 13 ya aina mahususi zinazotumikiwa katika elimu maalumu. Mahitaji ya kila kategoria yanaamliwa kwa mujibu wa sheria ya taifa au jimbo.

## *Programu ya Elimu Inayomlenga Mtoto (IEP)*

Wewe kama mzazi unasaidia kufanya maamuzi kuhusu elimu ya mtoto wako na kuwa mshirika wa timu na wafanyikazi wengine wa shule na wataalamu. Pamoja, mtaamua programu ya elimu ya mtoto wako ijulikanayo kama Elimu Inayomlenga Mtoto, au IEP. IEP ni mchakato na stakabadhi ambazo zinahitaji kuandikwa, kwa sababu inaelezea jinsi shule imepanga kumsaidia mtoto mtoto wako kuimarika na kujenga ujuzi kipindi chote cha mwaka.

## *Kuweka Anakofaa*

Baada ya timu kuamua ni huduma na usaidizi gani muhimu kwa mtoto, hatua inayofuata ni kuamua ni wapi huduma hizo zinafaa kutolewa. Hili linaitwa kuwekwa anakofaa. Mwanafunzi anafaa kuhudumiwa katika Mazingira Yasiyokuwa Yasiyokwaza Iwezekanavyo (LRE), yanayomfaa mtoto huyo.

## *Uhakiki wa Kila Mwaka*



Angalau mara moja kwa mwaka, timu itakutana kutathmini programu nzima ya mtoto na kusasisha malengo ya IEP. Kama itabainika kwamba mwanafunzi hahitaji elimu maalum, mtoto hataendelea na mchakato huo wa IEP na ataondoka katika hiyo programu.

## Haki za Kufuata Utaratibu

Una haki ya kutokubaliana na timu wakati wowote katika kipindi cha mchakato. Kama utatofautiana nayo, una chaguo la mchakato (kisheria) wa haki, ikiwemo upatanishi, uliofafanuliwa katika sheria. Haki hizi zimeelezwa kwa kina na zinapatikana katika hati ya haki

unayopewa na shule. Huu ni mhutasari mfupi sana wa mchakato wa elimu maalumu, na haujaelezea haki zako zote

## Je, Unahitaji Usadizi Zaidi?

Kwa miaka 37, wafanyikazi wa Utah Parent Center wamesaidia kubadilisha maisha ya watoto wenye ulemavu. Kama wazazi, tunaelewa jinsi inavyokaa na kuhisi kuwa na mtoto mwenye ulemavu. Sisi ni wazazi tunaowasaidia wazazi wengine kwa lugha zote mbili Kiingereza na Kihispania kote Katika Jimbo la Utah kwa kutoa warsha za bure, ushauri binafsi wa bure na maelezo ya kina- tunasaidia familia na watoto wao wenye mahitaji maalumu – kupata usaidizi wanaoihitaji.